

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) ULIOFANYIKA JUNI/JULAI 2020

Imetolewa na:

KATIBU MTENDAJI

21 AGOSTI, 2020

TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) ULIOFANYIKA JUNI /JULAI, 2020

1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **137** uliofanyika leo tarehe **21 Agosti 2020** katika Ukumbi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) - Zanzibar, Baraza la Mitihami la Tanzania limeidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Mitihami wa Kidato cha Sita (**ACSEE**) uliofanyika tarehe **29 Juni - 16 Julai, 2020**.

2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

2.1 Watahiniwa wote

Jumla ya watahiniwa **85,499** waliosajiliwa kufanya Mitihami wa Kidato cha Sita **Juni/Julai, 2020** wakiwemo wasichana **36,168 (42.30%)** na wavulana **49,331 (57.70%)**. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa wa Shule walikuwa **74,753** na watahiniwa wa kujitegemea walikuwa ni **10,746**.

Kati ya watahiniwa **85,499** waliosajiliwa kufanya Mitihami wa Kidato cha Sita **Juni/Julai, 2020**; watahiniwa **84,212** sawa na asilimia **98.49** walifanya mtihami na watahiniwa **1,287** sawa na asilimia **1.51** hawakufanya mtihami kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za Ugonjwa na Utoro.

2.2 Watahiniwa wa Shule

Kwa Watahiniwa wa Shule, kati ya watahiniwa **74,753** waliosajiliwa, watahiniwa **74,284** sawa na asilimia **99.37** walifanya mtihami ambapo wasichana walikuwa **32,403 (99.60%)** na wavulana **41,881 (99.19%)**. Watahiniwa **469 (0.63%)** hawakufanya mtihami.

2.3 Watahiniwa wa Kujitegemea

Kwa Watahiniwa wa Kujitegemea, kati ya watahiniwa **10,746** waliosajiliwa, watahiniwa **9,928** sawa na asilimia **92.39** walifanya mtihami na watahiniwa **818** sawa na asilimia **7.61** hawakufanya mtihami.

3.0 MATOKEO YA MTIHANI

3.1 Watahiniwa Wote

Jumla ya watahiniwa **82,440** sawa na asilimia **98.35** ya watahiniwa waliofanya Mitihami wa Kidato cha Sita **Juni/Julai,**

2020 wamefaulu. Wasichana waliofaulu ni **35,486** sawa na asilimia **99.07** wakati wavulana waliofaulu ni **46,954** sawa na asilimia **97.81**. Mwaka 2019 watahiniwa waliofaulu walikuwa **88,069** sawa na asilimia **98.32**.

3.2 Watahiniwa wa Shule

Watahiniwa wa Shule waliofaulu ni **73,537** sawa na asilimia **99.51** ya waliofanya mtihani. Wasichana waliofaulu ni **32,255** sawa na asilimia **99.68** na wavulana ni **41,282** sawa na asilimia **99.37**. Mwaka 2019 Watahiniwa **78,666** sawa na asilimia **99.14** ya Watahiniwa wa Shule walifaulu mtihani huo.

3.3 Watahiniwa wa Kujitegemea

Idadi ya Watahiniwa wa Kujitegemea waliofaulu mtihani ni **8,903** sawa na asilimia **89.71**. Mwaka 2019 Watahiniwa wa Kujitegemea **9,403** sawa na asilimia **91.95** walifaulu mtihani huo.

4.0 UBORA WA UFAULU

Ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata Watahiniwa wa Shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **72,230** sawa na asilimia **97.74** wamefaulu katika Daraja la I hadi III wakiwemo wasichana **31,786** sawa na asilimia **98.24** na wavulana **40,444** sawa na asilimia **97.35**.

Jedwali lifuatalo linaonesha ufaulu kwa kila Daraja kwa Watahiniwa wa Shule na kwa Jinsi:

Madaraja ya ufaulu	Wavulana		Wasichana		Jumla	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
I	6,638	15.98	4,709	14.55	11,347	15.35
II	20,004	48.15	16,771	51.83	36,775	49.76
III	13,802	33.22	10,306	31.85	24,108	32.62
I – III	40,444	97.35	31,786	98.24	72,230	97.74
IV	838	2.02	469	1.45	1,307	1.77
I – IV	41,282	99.37	32,255	99.68	73,537	99.51
O	262	0.63	102	0.32	364	0.49

5.0 UFAULU WA MASOMO KWA WATAHINIWA WA SHULE

Takwimu za ufaulu kwa watahiniwa wa Shule wa **ACSEE** Juni/Julai, 2020 zinaonesha kuwa ufaulu katika masomo ya **General Studies, History, Geography, Arabic Language, Physics, Chemistry, Biology, Agriculture, Basic Applied Mathematics, Advanced Mathematics, Economics, Commerce** na **Accountancy** umepanda ikilinganishwa na mwaka 2019. Ufaulu katika somo la **Kiswahili** ni asilimia 100 sawa na ufaulu wa somo hilo kwa mwaka 2019. Aidha, ufaulu katika masomo ya **English Language, French Language, Computer Science** na **Food and Human Nutrition** umeshuka kidogo ikilinganishwa na mwaka 2019. Mchanganuo wa ufaulu kwa kila somo umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

NA.	SOMO	2019	2020
		UFAULU (%)	UFAULU (%)
1.	GENERAL STUDIES	92.14	96.97
2.	HISTORY	98.91	99.65
3.	GEOGRAPHY	99.52	99.72
4.	KISWAHILI	100.00	100.00
5.	ENGLISH LANGUAGE	99.92	99.32
6.	FRENCH LANGUAGE	93.68	88.42
7.	ARABIC LANGUAGE	80.69	81.86
8.	PHYSICS	89.13	92.25
9.	CHEMISTRY	92.82	94.82
10.	BIOLOGY	96.12	96.99
11.	AGRICULTURE	98.49	98.73
12.	COMPUTER SCIENCE	94.29	82.05
13.	BASIC APPLIED MATHEMATICS	56.21	59.31
14.	ADVANCED MATHEMATICS	86.74	90.63
15.	ECONOMICS	98.25	99.28
16.	COMMERCE	99.88	99.93
17.	ACCOUNTANCY	96.08	98.66
18.	FOOD AND HUMAN NUTRITION	98.54	98.34

6.0 SHULE ZILIZOFANYA VIZURI ZAIDI

Ubora wa shule umepangwa kwa kutumia kigezo cha **Wastani wa Pointi (Grade Point Average – GPA)** kwa ufaulu wa shule kimasomo na kimadaraja. Mchanganuo wa Shule zilizofanya vizuri zaidi ni kama ifuatavyo:

6.1 Shule kumi (10) bora Kitaifa

NÁ	JINA LA SHULE	IDADI YA WATAHINIWA	MKOA	UMILIKI
1.	KISIMIRI	53	ARUSHA	SERIKALI
2.	KEMEBOS	37	KAGERA	BINAFSI
3.	AHMES	103	PWANI	BINAFSI
4.	MZUMBE	137	MOROGORO	SERIKALI
5.	TABORA GIRLS'	88	TABORA	SERIKALI
6.	TABORA BOYS'	96	TABORA	SERIKALI
7.	ILBORU	147	ARUSHA	SERIKALI
8.	KIBAHA	135	PWANI	SERIKALI
9.	MWANDET	43	ARUSHA	SERIKALI
10.	DAREDA	114	MANYARA	SERIKALI

6.2 Shule Kumi (10) zilizoongeza ufaulu kwa Miaka 3 Mfululizo

NA.	JINA LA SHULE	UMILIKI	MKOA	WASTANI WA GPA			% WASTANI WA KUPANDA
				2020	2019	2018	
1.	GOLDEN RIDGE	BINAFSI	GEITA	2.8333	3.1578	4.0428	16.09
2.	IGUNGA	SERIKALI	TABORA	2.3464	2.3911	3.3358	15.10
3.	DAREDA	SERIKALI	MANYARA	2.0295	2.1317	2.8533	15.05
4.	MACHAME GIRLS'	SERIKALI	KILIMANJARO	2.5496	2.9071	3.5315	14.99
5.	LIWALE DAY	SERIKALI	LINDI	2.4697	2.7168	3.3060	13.46
6.	NYANDUGA	SERIKALI	MARA	2.6170	2.6473	3.5515	13.31
7.	EDMUND-RICE-SINON	BINAFSI	ARUSHA	2.9243	3.0419	3.9272	13.20
8.	MKUGWA	SERIKALI	KIGOMA	2.5545	2.9333	3.3789	13.05
9.	RUHUWIKO	BINAFSI	RUVUMA	2.5483	2.8015	3.3608	12.84
10.	KILOSA	SERIKALI	MOROGORO	2.2257	2.2418	2.9859	12.82

6.3 Shule Kumi (10) zilizoshuka ufaulu kwa Miaka 3 Mfululizo

NA.	JINA LA SHULE	UMILIKI	MKOA	WASTANI WA GPA			% WASTANI WA KUSHUKA
				2020	2019	2018	
1.	DR. OLSEN	SERIKALI	MANYARA	3.3790	3.3307	2.6042	14.68
2.	MARIAN BOYS'	BINAFSI	PWANI	2.5435	2.3313	2.0128	12.46
3.	MPENDAE	SERIKALI	MJINI MAGHARIBI	4.7278	4.1984	3.7735	11.94
4.	AIRPORT	BINAFSI	MBEYA	3.5203	3.1219	2.8698	10.77
5.	SWILLA	BINAFSI	MBEYA	3.6591	3.3548	3.0537	9.47
6.	MAGUFULI	SERIKALI	GEITA	2.8292	2.3892	2.3841	9.32
7.	MUDIO ISLAMIC SEMINARY	BINAFSI	KILIMANJARO	3.0328	2.6063	2.5606	9.08
8.	KIBAKWE	SERIKALI	DODOMA	2.9279	2.5452	2.4722	9.00
9.	LUPA	SERIKALI	MBEYA	3.5365	3.0206	2.9953	8.96
10.	KIEMBESAMAKI 'A' ISLAMIC	SERIKALI	MJINI MAGHARIBI	4.6318	4.0510	3.9620	8.29

6.4 Mikoa Mitatu (03) iliyofanya vizuri zaidi

MKOA	IDADI YA SHULE	IDADI YA WATAHINIWA	NAFASI
LINDI	9	940	1
MTWARA	14	1,576	2
SIMIYU	10	955	3

6.5 Mikoa Mitatu (03) iliyoongeza Ufaulu kwa Miaka 3 mfululizo

MKOA	IDADI YA WATAHINIWA	% UFAULU			% WASTANI WA KUPANDA	NAFASI
		2020	2019	2018		
LINDI	940	2.7447	2.7992	3.1182	6.09	1
SIMIYU	955	2.8946	3.0043	3.2308	5.33	2
RUVUMA	3,282	2.9570	2.9617	3.2758	4.88	3

6.6 Mikoa Mitatu (03) iliyoshuka Ufaulu kwa Miaka 3 mfululizo

Hakuna

7.0 WATAHINIWA WALIOFANYA VIZURI ZAIDI KITAIFA

Watahiniwa waliofanya vizuri zaidi kitaifa wamepatikana kwa kulinganisha jumla ya pointi kwenye masomo ya **tahasusi** (combination) pamoja na wastani wa alama za jumla walizopata.

7.1 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	ALEX JOSEPH MBOGO	M	KIBAHA	PWANI	PCB
2.	LONGNUS GILBERTH MGAZA	M	ILBORU	ARUSHA	PCB
3.	CLAUD J KITUMBIKA	M	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
4.	MWESIGA C RWEGERERA	M	KISIMIRI	ARUSHA	PCM
5.	MARIA HEWA GAMBALOYA	F	MARIAN GIRLS'	PWANI	PCM
6.	MARIETHA PASTORY MONDEA	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
7.	ABUU HAMAD MTAMBO	M	KISIMIRI	ARUSHA	PCM
8.	ASTERIUS SALUM MAYAYA	M	MZUMBE	MOROGORO	PCM
9.	EDWARD L NDONYO	M	ILBORU	ARUSHA	PCM
10.	NISHA B NKYA	F	FEZA GIRLS'	DAR ES SALAAM	PCM

(a) Wasichana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	MARIA HEWA GAMBALOYA	MARIAN GIRLS'	PWANI	PCM
2.	MARIETHA PASTORY MONDEA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
3.	NISHA B NKYA	FEZA GIRLS'	DAR ES SALAAM	PCM
4.	CLARA FREDY MALANDO	TABORA GIRLS'	TABORA	PCB
5.	ELIZABETH MANGU	MARIAN GIRLS'	PWANI	PCM
6.	ROSEMARY L KILEMBE	FEZA GIRLS'	DAR ES SALAAM	PCM
7.	ANNA PETER MLAY	PANDAHILL	MBEYA	PCM
8.	ELIZABETH B KWAY	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
9.	ELIZABETH LUCAS NGWALU	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
10.	CAROLINA SIJAONA KABEBEKA	NGANZA	MWANZA	PCM

(b) Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	ALEX JOSEPH MBOGO	KIBAHA	PWANI	PCB
2.	LONGNUS GILBERTH MGAZA	ILBORU	ARUSHA	PCB
3.	CLAUD J KITUMBIKA	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
4.	MWESIGA C RWEGERERA	KISIMIRI	ARUSHA	PCM
5.	ABUU HAMAD MTAMBO	KISIMIRI	ARUSHA	PCM
6.	ASTERIUS SALUM MAYAYA	MZUMBE	MOROGORO	PCM
7.	EDWARD L NDONYO	ILBORU	ARUSHA	PCM
8.	AHAZI JAREDI	TABORA BOYS'	TABORA	PCM
9.	EMERSON FAUSTINE MAHUWI	MZUMBE	MOROGORO	PCM
10.	SAMWEL CHRISTOPHER MALEMBO	MZUMBE	MOROGORO	PCM

7.2 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	JOSEPH I MASANGULA	M	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
2.	NDUHIRUBUSA JAMALI JANUARY	M	MILAMBO	TABORA	KLF
3.	THEONTIUS RUTATOLA THEOBALD	M	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
4.	PRISCUS JOSEPH THOMAS	M	LYAMUNGO	KILIMANJARO	HGE
5.	MARIAM GODWIN KIMARIO	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGL
6.	ILONGA DESDERY SIGONDA	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGL
7.	ERASTO MUSA MAGAVILO	M	AHMES	PWANI	EGM
8.	STEPHEN LUHELO MLOGOLO	M	NDANDA	MTWARA	EGM
9.	DINA DAWSON RUGAIMUKAMU	F	ST.MARY GORETI	KILIMANJARO	EGM
10.	CUTHBERT LOPENY RAMAT	M	AHMES	PWANI	EGM

(a) Wasichana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	MARIAM GODWIN KIMARIO	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGL
2.	ILONGA DESDERY SIGONDA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGL
3.	DINA DAWSON RUGAIMUKAMU	ST.MARY GORETI	KILIMANJARO	EGM
4.	GLORIA STEPHEN VASONGA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGE
5.	MARY VICTOR CHAMI	TABORA GIRLS'	TABORA	HGL
6.	CATHERINE F WILLIAM	FEZA GIRLS'	DAR ES SALAAM	EGM
7.	REBEKA B MWAIBINGILA	PATRICK MISSION	DAR ES SALAAM	HGE
8.	ELIZABETH FELIX KIMARIO	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	HGE
9.	ESTHER CHARLES MABOJA	AHMES	PWANI	EGM
10.	ZAINABU HASSAN MAHUNGO	KISIMIRI	ARUSHA	HKL

Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	JOSEPH I MASANGULA	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
2.	NDUHIRUBUSA JAMALI JANUARY	MILAMBO	TABORA	KLF
3.	THEONTIUS RUTATOLA THEOBALD	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
4.	PRISCUS JOSEPH THOMAS	LYAMUNGO	KILIMANJARO	HGE
5.	ERASTO MUSA MAGAVILO	AHMES	PWANI	EGM
6.	STEPHEN LUHELO MLOGOLO	NDANDA	MTWARA	EGM
7.	CUTHBERT LOPENY RAMAT	AHMES	PWANI	EGM
8.	MJAHIDINA JUMA ALLY	KIGONSERA	RUVUMA	HGL
9.	ASHFAQ ASHRAF AHMED	KEMEBOS	KAGERA	EGM
10.	HAROLD BWIGA SANJA	BEREGE	DODOMA	HKL

7.3 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	SAMIYA SEIF ALLY	F	ST. CHRISTINA GIRLS'	TANGA	ECA
2.	AUGENIA D MSHAULA	F	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA
3.	MARINA FILBERT SOMOKA	F	PATRICK MISSION	DAR ES SALAAM	ECA
4.	SHEILA H NTISI	F	BAOBAB	PWANI	ECA
5.	TATU R KIKANDA	F	BENJAMIN WILLIAM MKAPA	DAR ES SALAAM	ECA
6.	SAADIA MEHBOOB YUSSUPH	F	SHAABAN ROBERT	DAR ES SALAAM	ECA
7.	KALUMUNA JOHNSON JOHN	M	KEMEBOS	KAGERA	ECA
8.	CONSOLATHA R MGINA	F	MRINGA	ARUSHA	ECA
9.	APAIKUNDA GODWISHES OLOTU	F	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA
10.	ABDULRAHMAN ABDALLAH MKANJIMA	M	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	ECA

(a) Wasichana kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	SAMIYA SEIF ALLY	ST. CHRISTINA GIRLS'	TANGA	ECA
2.	AUGENIA D MSHAULA	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA
3.	MARINA FILBERT SOMOKA	PATRICK MISSION	DAR ES SALAAM	ECA
4.	SHEILA H NTISI	BAOBAB	PWANI	ECA
5.	TATU R KIKANDA	BENJAMIN WILLIAM MKAPA	DAR ES SALAAM	ECA
6.	SAADIA MEHBOOB YUSSUPH	SHAABAN ROBERT	DAR ES SALAAM	ECA
7.	CONSOLATHA R MGINA	MRINGA	ARUSHA	ECA
8.	APAIKUNDA GODWISHES OLOTU	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA
9.	ZUBEDA BAKAR HEMED	CHASASA	KASKAZINI PEMBA	ECA
10.	RAYER JAMAL NASSORO	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA

(b) Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHENGO
1.	KALUMUNA JOHNSON JOHN	KEMEBOS	KAGERA	ECA
2.	ABDULRAHMAN ABDALLAH MKANJIMA	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	ECA
3.	ALBERT MWESA SUNGHWA	ST.JOSEPH'S CATHEDRAL	DAR ES SALAAM	ECA
4.	LADISLAUS A BUDILI	TUSIIME	DAR ES SALAAM	ECA
5.	RAJABU FADHIL MCHOMVU	KIBAHA	PWANI	ECA
6.	MUSSA S WILSON	BONDENI	ARUSHA	ECA
7.	ALLEN MUSHUMBUSI JONATHAN	KIBAHA	PWANI	ECA
8.	GODFREY ANSELIM ASSENKA	EAGLES	PWANI	ECA
9.	GRAYSON GODSON KIMARO	ST.MARY GORETI	KILIMANJARO	ECA
10.	SAMWEL GERALD NGOWI	ST.MARY GORETI	KILIMANJARO	ECA

8.0 TATHMINI YA AWALI YA MATOKEO

Takwimu za ufaulu wa Mithani wa Kidato cha Sita, 2020 zinaonesha kuwa shule zote nchini zimeendelea kufanya vizuri. Ufaulu wa jumla unaonesha kupanda kwa asilimia 0.03 ambapo mwaka 2019 ufaulu ulikuwa asilimia 98.32 na mwaka 2020 ufaulu ni asilimia 98.35. Aicha, ubora wa ufaulu umezidi kuimarika kwa kuwa idadi ya watahiniwa waliotafuuli vizuri katika daraja la I, II na III imeongezeka kwa asilimia 1.13 kutoka asilimia 96.61 mwaka 2019 na kuwa asilimia 97.74 mwaka 2020. Takwimu za matokeo zinaonesha pia kuwa ubora wa ufaulu wa wasichana kwa mwaka 2020 ni mzuri zaidi kuliko ule wa wavulana kwa asilimia 0.89.

Baraza la Mithani la Tanzania litafanya uchambuzi wa kina wa matokeo haya kwa kila somo na kutoa machapisho ya uchambuzi huo yatakayowasilishwa kwa wadau wa Elimu, zikiwemo shule zote za Sekondari za juu ('A' level) nchini kwa lengo la kuwawezesha walimu kutumia taarifa za uchambuzi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzani shuleni.

9.0 MATOKEO YA MITHANI YALIYOZULIWA

Baraza la Mithani la Tanzania limezua kutoa matokeo ya watahiniwa 22 wa shule ambao walipata matatizo ya kiatifa na kushindwa kufanya mihani kwa baadhi ya masomo. Watahiniwa husika wamepewa fursa ya kufanya Mithani wa Kidato cha Sita Mei, 2021, kama watahiniwa wa shule.

10.0 MATOKEO YA MTIHANI YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani la Tanzania limefuta matokeo yote ya watahiniwa watano (05) waliobainika kufanya udanganyifu katika mtihani. Kati ya watahiniwa hawa, wawili (02) ni watahiniwa wa shule na watatu (03) ni watahiniwa wa kujitegemea.

11.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Majiji nchini, Wakuu wa Shule na Wasimamizi wa Mitihani iliyofanyika Juni/Julai, 2020 kwa kuzingatia na kusimamia taratibu za Uendeshaji Mitihani na hivyo kuzuia kwa kiasi kikubwa udanganyifu kufanyika. Aidha, Baraza linawapongeza watahiniwa wote waliofanya Mtihani wa Kidato cha Sita, 2020 kwa kutojihusisha na udanganyifu.

12.0 KUANGALIA MATOKEO YA MTIHANI

Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) uliofanyika Juni/Julai, 2020 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- www.matokeo.necta.go.tz,
- www.necta.go.tz,
- www.tamisemi.go.tz,
- www.tanzania.go.tz


Dkt. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI
21/08/2020